

# MINUTE SHEET

8

DOKEZO  
No.

**KWENDA: KAIMU MKURUGENZI UWEZESHAJI UWEKEZAJI**

**KUTOKA: MENEJA KANDA-LAKE**

**TAREHE: 07//06/2021**

**YAH: TAARIFA FUPI KUHUSU MRADI WA TARIME WOOD  
AND POLES TREATMENT PLANT LIMITED**

Tumepokea maombi kutoka kampuni tajwa hapo juu ikiomba TIC iweze kutoa upya (re-issuance) cheti cha uwekezaji ambacho kilitolewa na TIC mwaka chenye namba ya usajili 042671 ya mwaka mwezi Mei 2014.

Tarime wood and poles treatment plant Limited ni moja ya miradi mikubwa tarajiwa ambayo inatarajiwa kuzalisha mbao kwa ajili ya nguzo za umeme na kuizuia TANESCO na mashirika mengine ya umeme ya Afrika Mashariki.

Mradi huu ulikwama kuanzishwa kutokana na kupungukiwa na mtaji ambao waliahidiwa awali na benki ya TIB lakini kutokana na uhitaji wa dhamana (collateral) nyingi walishindwa kupata mtaji wa kuendeleza mradi huo.

Mradi huo kwa sasa umepata Mbia kutoka Kenya Kampuni ya Truck City Limited ambapo katika makubaliano atawekeza katika machine na Tarime wood itawekeza katika ujenzi wa kiwanda na kuchangia sehemu kubwa ya miti ambayo itachatwa ambapo shamba lipo na miti ipo tayari kuvunwa.

# MINUTE SHEET

DOKEZO  
No.

Hivyo basi nashauri waweze kupata cheti kingine cha uwekezaji kwa sababu zifuatazo;

Mradi huo kwa sasa upo tayari kuanza na hakuna mabadiliko kwenye maeneo yafuatayo;

- i. Mradi bado upo kwenye eneo lile lile la awali
- ii. Mradi haujabadilisha jina wala wamiliki
- iii. Mradi unaomba cheti ili uendelezwa na haujabadilisha mtaji uliowasilishwa kwenye mchanganuo hapo awali.
- iv. Ni mradi ambao utanzishwa na kufanya kazi haraka iwapo tutaupa ushirikiano.
- v. Mradi haujawahi kutumia vivutio vilivyotolewa awali na TRA kama ilivyoambatanishwa hivyo basi tunawaomba waweze kupata uli waweze kutumia

Nawasilisha kwa hatua zaidi;

Pendo Gondwe



Meneja Kanda ya Ziwa